



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



Unapojibu tafadhali taja:

KUMB.NA.NA. IMC/F.20/27/78

11 Agosti, 2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ANAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI ZA MUDA KUTOKA KWA WATANZANIA WENYE SIFA NA UWEZO WA KUJAZA NAFASI ZA KAZI YA MUDA KAMA ZILIVYOAINISHWA KWENYE TANGAZO HILI.

1. AFISA TEHAMA MSAIDIZI - (NAFASI 1)

SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wenye Elimu na Cheti cha Kidato cha nne (IV) au sita (VI) waliohitimu mafunzo ya **Stashahada ya NTA Level 6** katika fani ya Sayansi ya Kompyuta (Diploma in Computer Science) Kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali: -

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kufanya Ukaguzi wa "Units" wa vifaa vya TEHAMA na kurekebisha ipasavyo.
- ii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya vifaa vya TEHAMA.
- iii. Kufanya matengenezo ya miundombinu ya TEHAMA.
- iv. Kuchukua hatua za kiusalama kulinda vifaa vya TEHAMA
- v. Kukagua na kutambua vifaa vinavyohitaji matengenezo.
- vi. Kusimamia ukaguzi na ufungaji wa vifaa vipya vya TEHAMA.
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Msimamizi wake.

ii

iii

iv

v

vi

vii

1





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



Unapojibu tafadhali taja:

KUMB.NA.NA. IMC/F.20/27/78

11 Agosti, 2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ANAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI ZA MUDA KUTOKA KWA WATANZANIA WENYE SIFA NA UWEZO WA KUJAZA NAFASI ZA KAZI YA MUDA KAMA ZILIVYOAINISHWA KWENYE TANGAZO HILI

1. AFISA TEHAMA MSAIDIZI - (NAFASI 1)

SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wenye Elimu na Cheti cha Kidato cha nne (IV) au sita (VI) waliohitimu mafunzo ya **Stashahada ya NTA Level 6** katika fani ya Sayansi ya Kompyuta (Diploma in Computer Science) Kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali: -

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kufanya Ukaguzi wa "Units" wa vifaa vya TEHAMA na kurekebisha ipasavyo.
- ii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya vifaa vya TEHAMA.
- iii. Kufanya matengenezo ya miundombinu ya TEHAMA.
- iv. Kuchukua hatua za kiusalama kulinda vifaa vya TEHAMA
- v. Kukagua na kutambua vifaa vinavyohitaji matengenezo.
- vi. Kusimamia ukaguzi na ufungaji wa vifaa vipya vya TEHAMA.
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Msimamizi wake.

1

11/8/2022

2. FUNDI SANIFU (UMEME) - (NAFASI 1)

SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wenye Elimu na Cheti cha Kidato cha nne (IV) au sita (VI) waliohitimu mafunzo ya **stashahada ya NTA Level 6** katika Fani ya "Electrical" au "Full Technician Certificate" kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali: -

MAJUKUMU YA KAZI

Kufanya matengenezo ya vifaa vya umeme na mifumo yote ya umeme.

- i. Kusimika mifumo ya umeme kama ilivyoelekezwa katika michoro.
- ii. Kufanya majaribio (testing) ya mara kwa mara katika vifaa vya umeme.
- iii. Kufanya ukaguzi katika mifumo na vifaa vya umeme.
- iv. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

3. MHUDUMU WA OFISI - (NAFASI 1)


SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wenye Elimu na Cheti cha Kidato cha nne na kuendelea

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kufanya usafi wa Ofisi na Mazingira ya nje na ya ndani ikiwa ni pamoja na kufagia, kufuta vumbi, kupiga deki, kufyeka majani, kupalilia bustani, kupanda maua na kusafisha vyoo.
- ii. Kuchukua na kupeleka majalada na hati nyingine kwa maofisa wanaohusika na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- iii. Kusambaza barua za ofisi kwa jinsi atakavyoelekezwa.
- iv. Kutayarisha chai ya Ofisi
- v. Kuhakikisha kuwa vifaa vya Ofisi vinawekwa sehemu zinazostahili
- vi. Kufungua milango na madirisha ya Ofisi wakati wa Asubuhi na kufunga baada ya saa za kazi (jioni).

2


MKURUGENZI HALMASHAURI YA
S.L.P. 735
MWANZA.
MANISPAA YA ILEMELA

- vii. Kudurufu barua au machapisho kwenye mashine za kudurufia
- viii. Kutunza vifaa vya ofisi na kutoa ripoti kila vinapoharibika.

Kufanya kazi nyingine atakazoelekezwa na Msimamizi wake.

4. VIBARUA WA KUKUSANYA MAPATO - (NAFASI 18)

SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wenye Elimu na Cheti cha Kidato cha nne (IV) na kuendelea.

MAJUKUMU YA KAZI


- i. Kukusanya Mapato kutoka kwenye vyanzo atakavyopangiwa kukusanya
- ii. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yaliyokusanywa kwa siku hiyo yanawekwa benki.
- iii. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yanakusanywa kwa kutumia "POS Machines" na kutoa risti halali za Halmashauri kwa makusanyo yaliyokusanywa.
- iv. Kuhakikisha kuwa "POS Machines" zinakuwa katika hali nzuri na zinatumika muda wote.
- v. Kufanya kazi nyingine atakazoelekezwa na Msimamizi wake wa kazi.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne au cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho.
- v. "Testimonials", "Provisional Results", "Statements of Results", hati matokeo za kidato cha nne au cha sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**

3


11/8/2022



- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- viii. **Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 18 AGOSTI, 2022 saa 9.30 Alasiri.**
- ix. Barua za maombi ya kazi ziandikwe **kwa Mkono** na kutumwa au kufikishwa Masjala ya Wazi ya Mkurugenzi kwa anwani ifuatayo: -

**MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA,
S.L.P 735,
MWANZA.**

LIMETOLEWA NA;


Eng. Modest J. Apoloni
**MKURUGENZI WA MANISPAA
ILEMELA**

